

RC CHALAMILA AZUNGUMZA NA WANANCHI WA IBWERA BUKOBA

Na. Milka Kaswamila- Bukoba DC

Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mheshimiwa Albert Chalamila, akiwa ameambatana na Kamati ya Usalama ya Mkoa huo pamoja Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, amekemea vikali tabia ya baadhi ya wazazi kuwaficha watoto wao ili wasiendelee na masomo ya elimu ya sekondari na kuwataka wazazi kwa ujumla wao watambue kwamba chakula mashuleni sio mchango bali ni hitaji la msingi kwa mtoto hivyo wahakikishe wanachangia upatikanaji wa huduma hiyo ili watoto waweze kusoma vizuri na kupata ufaulu mzuri katika masomo yao.

Mheshimiwa Chalamila amesema hayo wakati alipokuwa akizungumza na hadhara ya kata ya Ibwera ndani ya Halmashauri ya Wilaya Bukoba na kusisitiza kwamba, mzazi ambaye atabainika kumficha mtoto wake au kumzuia kwa namna yoyote ile asiende shule, atachukuliwa hatua kali za kisheria.



“Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imejenga vyumba vya madarasa katika shule za kata nchi nzima na kuondoa karo ili watoto waweze kupata elimu itakayowasaidia kuboresha hali ya maisha yao binafsi na jamii kwa ujumla, kwa hiyo wazazi na walezi hakikisheni mnawapeleka watoto shule na kuwapa mahitaji yao ya msingi zikiwemo sare za shule na chakula” alifafanua Mheshimiwa Chalamila.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, Bi. Fatina Hussein Laay, akatumia mkutano huo kukazia masuala ya lishe kwa wajawazito na watoto hasa wa umri wa chini ya miaka mitano, ulinzi wa mtoto na athari za matumizi ya dawa za kienyeji za kuchochea uchungu kwa wanawake wajawazito.

“Wanawake wenzangu, acheni matumizi ya dawa zenu za asili za kuchochea uchungu kwani wakati mwingine zinapelekea kupasuka kwa nyumba ya uzazi na kusababisha vifo vya wajawazito na watoto. Lakini pia mnapowazaa watoto, hakikisheni mnawapa lishe bora ili wasidumae na muwalinde dhidi ya ukatili ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama endapo mtoto au hata mtu mzima atabainika kufanyiwa ukatili wa namna yoyote ile” alisisitiza Fatina.



Aidha, katika mkutano huo wananchi walishukuru sana kwa ujio wa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwenye kata yao na wakaomba wasaidiwe kutatuliwa changamoto za barabara na umeme na mwakilishi wa wazee akaomba kuwepo na kliniki tembezi itakayokuwa na wataalamu wa magonjwa ya wazee ili kurahisisha upatikaji wa huduma za afya kwa kundi hilo maalum katika jamii na nchi kwa ujumla.



Mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye kata ya Ibwera ulitanguliwa na taarifa kutoka kwa diwani wa kata hiyo, Mheshimiwa Michael Lubisi ikipongeza utekelezaji wa miradi ya elimu, afya, maji, kilimo na barabara ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekwisha kufanya na inaendelea kufanya ndani ya kata hiyo.



MWISHO